


WIZARA YA AFYA

OFISI YA RAIS – TAWALA

ZA MIKOA NA SERIKALI

ZA MITAA

**MWONGOZO WA KUENZISHA BODI ZA
AFYA ZA HALMASHAURI**



YALIYOMO

SURA	UKURASA
<i>Dibaji</i>	(v)
<i>Shukrani</i>	(vii)
Vifupisho	(viii)
1. Sababu za kuundwa kwa Bodi za Huduma za Afya ya Halmashauri na Kamati za Usimamizi za Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati	1
1.1 Utangulizi	1
1.2 Misingi ya kisheria inayotumika kuunda Bodi za Afya za Halmashauri na Kamati za Vituo vya Huduma	2
2.0 Bodi ya Huduma Afya ya Halmashauri	3
2.1 Wajumbe wa Bodi	3
2.2 Sifa za wajumbe	3

2.3	Utaratibu wa uchaguzi	4
2.4	Uhusiano wa Bodi na Jamii, Washika Dau na Mamlaka zingine				5
2.5	Usimamizi wa rasilimali	6
2.6	Majukumu ya Bodi	8
2.7	Kazi za Bodi	8
2.8	Uwajibikaji	9
2.9	Uhalali wa kisheria, mamlaka na mipaka ya Bodi			9
2.10	Utaratibu wa kupokea na kutoa taarifa	10
3.0	Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri			12
3.1	Wajumbe wa Timu watakuwa kama ifuatavyo			...	12
3.2	Sifa za Wajumbe wa Kamati	12
3.3	Taratibu za Uchaguzi/Uteuzi	12
3.4	Uhusiano kati ya Jamii, Washika dau na Mamlaka zingine			...	12
3.5	Usimamizi wa Rasilimali	13
3.6	Majukumu na Kazi za Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri	13
3.7	Uwajibikaji	14
3.8	Uhalali wa Kisheria, Mamlaka na Mipaka	14
3.9	Mikataba ya Fedha	15
3.10	Utaratibu wa Kupokea na Kutoa Taarifa	15
4.0	Kamati ya usimamizi ya Hospitali	16
4.1	Wajumbe wa kamati	16
4.2	Sifa za wajumbe	17
4.3	Utaratibu wa uchaguzi	17
4.4	Uhusiano wa kamati na Jamii, Washika dau na Mamlaka zingine	18
4.5	Usimamizi wa rasilimali	19
4.6	Majukumu ya kamati	20

4.7	Kazi za kamati	20
4.8	Uwajibikaji	21
4.9	Uhalali wa kisheria, Mamlaka na Mipaka ya Kamati	21
4.10	Mikataba ya fedha	22
4.11	Utaratibu wa kupokea na kutoa Taarifa	22
5.0	Kamati ya Kituo cha Afya	23
5.1	Wajumbe wa kamati	23
5.2	Sifa za wajumbe wa kamati	23
5.3	Utaratibu wa uchaguzi wa wajumbe	24
5.4	Uhusiano wa kamati na Jamii, Washika dau na Mamlaka zingine	25
5.5	Usimamizi wa rasilimali	26
5.6	Majukumu ya kamati	27
5.7	Kazi za kamati	27
5.8	Uwajibikaji	28
5.9	Uhalali wa kisheria, Mamlaka na Mipaka ya Kamati	28
5.10	Mikataba ya fedha	29
6.0	Kamati ya Afya ya Kata	30
6.1	Wajumbe wa Kamati	30
6.2	Sifa za wajumbe.....	30
6.3	Taratibu za Uchaguzi	31
6.4	Uhusiano wa Kamati na jamii, Washikadau na Mamlaka zingine				31
6.5	Usimamizi wa Rasilimali	31
6.6	Kazi	31
6.7	Uwajibikaji	32
6.8	Uhalali wa Kisheria, Mamlaka na Mipaka ya Kamati	32
6.9	Utaratibu wa kupokea na kutoa taarifa	32

7.0	Kamati ya Zahanati	33
7.1	Wajumbe wa kamati		33
7.2	Sifa za wajumbe	33
7.3	Taratibu za uchaguzi	34
7.4	Uhusiano wa kamati na Jamii, Washika Dau na Mamlaka zingine...				34
7.5	Usimamizi wa rasilimali	35
7.6	Majukumu ya Kamati	36
7.7	Kazi za kamati	36
7.8	Uwajibikaji	37
7.9	Uhalali wa kisheria, Mamlaka na Mipaka	37
7.10	Mikataba ya fedha	38
8.0	Viambatanisho:	1
8.1	Kiambatanisho Na. 1	1
8.2	Kiambatanisho Na. II	2
8.3	Kiambatanisho Na. III	3
8.4	Kiambatanisho Na. IV	5

DIBAJI

Tangu Azimio la Alma Ata la Mwaka 1978, lilipotangazwa, iliazimiwa kuwa Huduma za Afya ya Msingi ziwe ndizo nguzo katika kuleta maendeleo ya afya. Jambo hili lilipitishwa na Baraza la Afya la Dunia kama mkakati wa kufikia lengo la Afya kwa wote..

Mwaka 1983, Wizara ya Afya ilitoa mwongozo wa utekelezaji wa Huduma za Afya ya Msingi nchini. Ili kufanikisha utekelezaji, mwongozo ulitaja mahitaji muhimu ya Afya ya Msingi kuwa ni:

1. Ushirikishwaji wa jamii
2. Ushirikiano na Sekta zingine
3. Kutoa madaraka kwa mikoa na wilaya
4. Usawa (uwezo wa kupata, kukubalika na kumudu)

Kwa hiyo, Huduma ya Afya ya Msingi ina vipengele vinne ambavyo ni muhimu kwa maendeleo ya afya ya jamii, na jambo hili litakuwa na maana tu endapo vipengele hivyo vitaimarishwa, kuendelezwa na kuwepo wakati wote. Vipengele hivyo ni:-

- (i) Huduma za Afya za Kinga
- (ii) Huduma za afya endelevu
- (iii) Huduma za Maendeleo ya Watumishi wa Afya
- (iv) Huduma za afya za tiba

Vipengele hivyo vinne vinaweza kutumika kama msingi imara utajengwa kwa kupitia ushirikishwaji wa kweli wa jamii ambao hatimaye utawezesha jamii kumiliki huduma hizo.

Umilikaji wa huduma kwa jamii utawawezesha watu kuwa na sauti, pamoja na kuhoji namna rasilimali za afya na huduma za afya zinavyosimamiwa. Hata hivyo, ili kuendeleza kiwango cha uwajibikaji cha jamii, juu ya mwendelezo wa huduma za afya, Shirika la Afya Duniani la Kuhudumia Watoto (UNICEF) lilitangaza Azimio la Bamako la mwaka 1987 ambalo linasema “kuwa na uwezekano wa kupata Huduma za Afya ya Msingi, zinazoendelezwa kwa kupitia njia ya kutoa madaraka zaidi ya maamuzi ya afya katika ngazi ya wilaya. Jamii kuendesha shughuli za Huduma za Afya ya Msingi, ugharamiaji wa huduma chini ya udhibiti wa jamii na sera ya kweli ya kitaifa ya dawa na utoaji wa dawa muhimu, inayolenga katika Huduma za Afya ya Msingi zinazojitosheleza na kwamba mkazo ukiwa katika kuendeleza afya ya kinamama na watoto”.

Hata hivyo, Azimio la Bamako pamoja na maazimio msunga mengine hayakuweza kufanikiwa kuleta Huduma za Afya ya Msingi endelevu katika vipengele vyake hivyo. Wakati huo huo, kuanguka kwa uchumi wa dunia na vita baina ya mataifa mbalimbali viliathiri uchumi na utendaji wa Tanzania katika sekta zote ikiwemo Sekta ya Afya. Mwaka 1997, Wizara ya Afya kwa msaada wa Benki ya Dunia, ilipitia upya utendaji wa Sekta ya Afya ambao ulionyesha kutokuwa na ufanisi, nafasi, ubora na ukosefu wa uwajibikaji katika muundo na rasilimali za fedha zisizotosheleza.

Ili kushughulikia mambo yaliyojitokeza kutokana na mapitio hayo na kuboresha matokeo ya huduma za afya katika kutoa matokeo mazuri ya afya, Wizara ya Afya ilitengeneza utaratibu wa Mabadiliko katika Sekta ya Afya. Katika hatua za awali, mtazamo wake uliwekwa katika

Mapendekezo ya Mabadiliko katika Sekta ya Afya (Desemba, 1994), na kutafsiriwa katika mtitiririko wa mipango ya miaka mitatu mitatu ili kutekeleza mapendekezo ya mabadiliko hayo.

Mkakati mkuu wa mabadiliko haya ni kurejesha madaraka ya uendeshaji huduma katika halmashauri na katika ngazi ya chini kabisa ya jamii kwa kuanzisha Bodi za Afya na Kamati za Afya za Vituo vya Huduma. Kwa kupitia muundo huu wa vyombo hivi katika jamii na marekebisho ya kutoa muundo wa vyombo hivi katika jamii na marekebisho ya kitaasisi, madaraka ya kweli ya jamii yataweza kupatikana.

Bodi hizi za Afya na Kamati za Afya za Vituo vya Huduma zitafanya kazi chini ya Halmashauri za Serikali za Mitaa.

Mpangilio huu mpya unahitaji mafunzo kwa Halmashauri, watumishi wa afya ya jamii, na hivyo umuhimu wa kijitabu hiki. Kijitabu hiki ni jaribio la kupata namna ya Mabadiliko yenyewe katika hali ambayo itawezesha kuwepo kwa kujiamini kwa jamii yenyewe kwa njia ya amani.

Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zinawatakiwa kila la kheri kwa wale wote watakao kitumia kijitabu hiki, katika kufanisha uundwaji wa Bodi na Kamati za Huduma za Afya nchini kote.

Mh. Anna M. Abdallah (MP)
WAZIRI WA AFYA

Mh. Hassan Ngwilizi (MP)
**WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA
MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

SHUKRANI

Kukamilika kwa mwongozo huu wa uanzishaji na uendeshaji wa Bodi za Afya za Halmashauri na kamati za afya za vituo vya huduma ni matokeo ya jitihada kubwa na kujitolea kwa watu na taasisi mbalimbali.

Wizara ya Afya na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zinathamini mchango wa wahisani kwa sekta ya afya wa kuanzisha mfuko wa pamoja ambao umechangia fedha zilizowezesha mwongozo huu kutayarishwa. Hata hivyo, siyo rahisi kuwataja wote waliochangia katika utengenezaji wa mwongozo huu, lakini uzoefu mkubwa uliopatikana kutoka sehemu za majaribio ya Mabadiliko katika Sekta ya Afya - Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) – Igunga, Mipango na Uendeshaji – Dodoma, Tunduru, Sengerema, Bunda, Bodi za Afya za Wilaya Kagera, Tanga na Dar es Salaam umetupatia mwelekeo wa namna ya kuishirikisha jamii katika kufanya maamuzi, kupanga na kuendesha shughuli za afya.

Hivyo, Wizara ya Afya inathamini mchango uliotokana na uzoefu mkubwa wa mkoa wa Kagera uliopatikana kwa msaada wa Shirika la Maendeleo la Denmark (DANIDA), mkoa wa Mbeya kupitia msaada wa Idara ya Maendeleo ya Serikali ya Uingereza (DFID), Mkoa wa Tanga kupitia msaada wa DHSP – GTZ, Dar es Salaam kupitia msaada wa SDC. CHF kupitia msaada wa Benki ya Dunia, kupanga na kuendesha – CSSC kupitia msaada wa GTZ na KFW. Wizara ya Afya na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pia inawashukuru wataalamu wa vitengo na Idara za Wizara ya Afya na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambao wameshiriki wakati wote wa kutengeneza kijitabu hiki. Sekretarieti ya Huduma za Afya ya Msingi ilitayarisha kazi hii kwa wakati na mwishowe kuwasilisha mwongozo huu wa uanzishaji na utendaji wa Bodi na kamati za huduma za afya.

Wizara ya Afya na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) inarudia kuwashukuru washiriki wote na watu binafsi kwa mchango yao ya mawazo na rasilimali zingine iliyowezesha kupatikana kwa sera ya kisekta.

Kwa namna ya pekee, Wizara ya Afya na Wizara ya TAMISEMI inajali na kuthamini mchango ya mawazo na kujitolea kwa dhati kwa wataalamu ambao wameonyeshwa Kiambatisho III ambao kwa pamoja wamechangia mawazo yao na kujitolea kwao kwa dhati kukamilisha mwongozo huu.

Akhsanteni

M.J. Mwaffisi
KATIBU MKUU
WIZARA YA AFYA

D.M.S. Mmari
KATIBU MKUU
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA
MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

VIFUPISHO

CHF	: Community Health Fund
DANIDA	: Danish International Development Agency
DFID	: Department For International Development
DHSP	: District Health Support Project
GTZ	: Deutsche Gessellschaft fur Technische Zusammenarbeit
SDC	: Swiss Development Corporation
CSSC	: Christian Social Services Commission
KFW	: Kreditanstalt Fur Wiederaufbau
TAMISEMI	: Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

SABABU ZA KUUNDWA KWA BODI ZA HUDUMA ZA AFYA ZA HALMASHAURI NA KAMATI ZA USIMAMIZI ZA HOSPITALI, VITUO VYA AFYA NA ZAHANATI

1.0 UTANGULIZI:

Mwaka 1993, Wizara ya Afya ikishirikiana na Wizara zingine, ilifanya mapitio ya Sekta ya Afya na ikapendekeza kufanyike Mabadiliko ya Sekta hiyo nchini. Mabadiliko haya yalianza mwaka 1994. Hii ilileta mtazamo mpya ambao ulianzisha mabadiliko yanayoendelea hivi sasa katika Sekta ya Afya yenye lengo la kuimarisha utekelezaji wa mkakati wa huduma za afya ya msingi.

Hali kadhalika, mapendekezo ya Mabadiliko ya Sekta ya Afya, yalibainisha maeneo ambayo yalihatiji kuongezewa nguvu au kupitiwa upya kwa lengo la kuboresha afya na utoaji wa huduma nchini. Ingawa utekelezaji wa mabadiliko haya unahitaji msaada kutoka nje, msaada huo utaelekezwa zaidi katika shughuli zitakazoweza mfumo wa utoaji wa huduma za afya kuwa wa kujitegemea na endelevu.

Mfumo na utekelezaji wa Mabadiliko ya Sekta ya Afya unaendana na Mabadiliko ya Serikali za Mitaa ambayo kwa pamoja yanalenga katika kuboresha utoaji wa huduma za afya kwa njia zifuatazo:-

- Kuziongezea Halmashauri madaraka na uwezo wa kuamua;
- Kuhamasisha na kushirikisha jamii na kaya katika kubuni, kupanga, kutekeleza na kutathmini mipango ya afya;
- Kuanzisha na kusimamia vyanzo vingine vya mapato kama vile Mfuko wa Afya ya Jamii, Uchangiaji Huduma za Afya na Bima ya Afya ambavyo vitasaidia kupunguza pengo la mapato lililopo katika Sekta ya Afya;
- Kuzipitia na kuzirekebisha kanuni, sheria na taratibu mbalimbali zinazohusu na uendeshaji huduma za afya nchini ili ziende na wakati.

Kwa kuunda Bodi za Huduma za Afya za Halmashauri na Kamati za Afya za Vituo vya Huduma, hatua za kufanikisha kuwepo kwa miundo ya kijamii na mipangilio ya kitaasisi ambayo itaongeza madaraka ya maamuzi ya kiutendaji kwa jamii zitafikiwa. Uundaji wa Bodi za Huduma za Afya za Halmashauri na Kamati za Afya za Vituo kutafanikisha kuwepo kwa miundo ya kijamii na kitaasisi ambayo itaongeza madaraka na mamlaka ya jamii juu ya uendeshaji huduma za afya.

1.2 Misingi ya kisheria itakayotumika kuunda Bodi za Huduma za Afya za Halmashauri na Kamati za Vituo vya Huduma

Sheria ya Serikali za Mitaa (Halmashauri za Wilaya) Na. 7 ya Mwaka 1982

- “Halmashauri ya Wilaya, kwa lengo la kutekeleza majukumu yake, inaweza kuunda Bodi kwa lengo la kutoa huduma ndani ya mipaka yake ya kisheria baada ya kutangazwa rasmi kwenye Gazeti la Serikali” (Kifungu cha 86 A - Bodi ya Huduma).
- “Kila Bodi ya Huduma itawajibika kwa Halmashauri ya Wilaya na itatekeleza kazi na majukumu yake kama itakavyoelezwa katika taratibu za kuundwa kwake
- “Madaraka ya Halmashauri ya Wilaya katika kutunga sheria ndogo ndogo” (kifungu cha 148).
- “Madaraka ya Mamlaka ya Miji katika kutunga sheria ndogo ndogo” (kifungu cha 155).

Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka ya Miji) ya Mwaka 1982.

- “Mamlaka ya Miji, kwa lengo la kutekeleza majukumu yake katika eneo lake, inaweza kuunda Bodi hizo za Huduma kama itakavyoona inafaa, baada ya kutolewa tangazo kwenye Gazeti la Serikali” (Kifungu cha 52A – Bodi ya Huduma).
- “Kila Bodi ya Huduma itawajibika kwa Halmashauri na itatekeleza kazi na majukumu yake kama itakavyoelezwa katika taratibu za kuundwa kwake”
- “Madaraka ya Mamlaka ya Halmashauri kuunda sheria ndogo ndogo”(Kifungu cha 80}
- “Muundo na kipindi cha uwakilishi vitakuwa kama itakavyoamuliwa na Halmashauri kwa kuzingatia taratibu za kuunda mamlaka yeyote”. (Kifungu cha 86 A na 52A – 1999).

2.0 BODI YA HUDUMA ZA AFYA YA HALMASHAURI

2.1 WAJUMBE WA BODI

2.1.1 Wajumbe wa Bodi ya Huduma za Afya za Halmashauri watakuwa katika makundi mawili:-

▪ **Wajumbe wa kuchaguliwa (wanaopiga kura)**

- Wawakilishi wa watumiaji huduma za afya (Jamii) wanne kati yao wawili ni wanawake 4
- Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii 1
- Mwakilishi kutoka watoa huduma za afya binafsi kwa faida 1
- Mwakilishi kutoka watoa huduma za afya binafsi bila faida 1

▪ **Sekretarieti (Wasiopiga kura)**

- Mganga Mkuu wa Halmashauri..... 1
 - Mwakilishi kutoka hospitali ya Halmashauri 1
 - Afisa Mipango wa Halmashauri..... 1
 - Mwakilishi kutoka Timu ya Uendeshaji Huduma za Afya ya Mkoa 1
- Jumla ya wajumbe 11**

Kumbuka:

- Mwenyekiti atatokana na wajumbe wa kuchaguliwa kwa kupigiwa kura.
- Mganga Mkuu wa Wilaya/Manispaa/Jiji atakuwa Katibu
- Wajumbe wengine wataalikwa kama kutakuwa na ulazima.

2.2 SIFA ZA WAJUMBE

Sifa za wajumbe wa Bodi zitazingatia mambo yafuatayo:-

2.2.1 Umri

Kwa kuzingatia majukumu ya wajumbe wa Bodi, umri unaopendekezwa ni kati ya miaka 25 - 70.

2.2.2 Uraia

Mjumbe wa Bodi atalazimika kuwa raia wa Tanzania. Sharti hili si la lazima kwa wajumbe kutoka Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

2.2.3 Elimu

Waombaji wanatakiwa wawe wamehitimu elimu ya sekondari na kuendelea.

***Kumbuka:* Itikadi ya kisiasa.**

Wajumbe wote saba wa kuchaguliwa isipokuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, **hawatakiwi** kuwa na nyadhifa zozote za kisiasa kwenye chama chochote cha siasa wala kuwa waajiriwa wa Halmashauri husika.

2.3 TARATIBU ZA UCHAGUZI

2.3.1 Uhamasishaji

Uhamasishaji kwa ajili ya uanzishaji wa Bodi za Huduma za Afya za Halmashauri na Kamati za Vituo vya Huduma, ni budi ushirikishe viongozi wa Halmashauri, na wananchi kwa jumla katika ngazi za wilaya au miji au Manispaa au Jiji, Kata, Vijiji na Mtaa. Madhumuni ya uhamasishaji huu ni kukuza ushirikishwaji wa jamii.

2.3.2 Halmashauri kutoa matangazo ya nafasi za Bodi/Kamati

Mkurugenzi wa Halmashauri atatangaza nafasi wazi kwa ajili ya uwakilishi wa hospitali, vituo vya afya na zahanati. Pia atahakikisha kwamba Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na watoa huduma binafsi wanajiunga katika vikundi ili wawe na uwakilishi kwenye Bodi na Kamati za Afya.

2.3.3 Uchaguzi wa Awali

Maombi na uchaguzi wa wajumbe utafanyikia kwenye kijiji au mtaa na kusimamiwa na Afisa Mtendaji wa Kijiji katika Halmashauri ya Wilaya au Afisa Mtendaji wa Kata katika Halmashauri ya Mji/Manispaa/Jiji. Uchaguzi utafanyika kwa njia ya mkutano wa hadhara na atachaguliwa mjumbe mmoja.

2.3.4 Uchambuzi wa maombi

Orodha ya wajumbe waliochaguliwa itapelekwa kwa Kamati ya Maendeleo ya Kata kwa uchambuzi wa awali na baadaye mapendekezo kupelekwa kwa Mkurugenzi wa Wilaya au Manispaa au Mji au Jiji.

2.3.5 Uchaguzi wa mwisho wa wajumbe wa Bodi

Uchaguzi Mkuu wa wajumbe waliochaguliwa kutoka kila kijiji/mtaa utafanywa na kikao kikuu cha Halmashauri kupitia Kamati ya Huduma za Jamii baada ya kupendekezwa na Timu ya Uendeshaji ya Halmashauri.

2.3.6 Uzinduzi rasmi

Bodi za Huduma za Afya za Halmashauri zitazinduliwa rasmi kwa ushuhuda wa Mkuu wa Wilaya baada ya kuidhinishwa na Kikao cha Halmashauri husika.

2.4 UHUSIANO KATI YA BODI NA JAMII, WASHIKA DAU NA MAMLAKA ZINGINE

2.4.1 Uhusiano na Jamii

- Bodi ya Huduma ya Afya ya Halmashauri itahakikisha kuwa jamii inashirikishwa kikamilifu katika kutambua matatizo, kuweka kipaumbele, kupanga, kuchangia huduma, kufuatilia na kutathmini utoaji wa huduma za afya;
- Bodi itahakikisha jamii inakuwa na uwezo wa kusimamia huduma za afya.

2.4.2 Uhusiano na Kamati za Vituo vya Huduma

- Kamati za Vituo vya Huduma zitawasilisha taarifa za fedha na utekelezaji za kila robo mwaka, na taarifa za mwaka kwa Bodi ya Huduma ya Afya ya Halmashauri.

2.4.3 Uhusiano na Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri

Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri kama ilivyonukuliwa katika ikama ya Watumishi ya Mwaka 1999 na kurekebishwa mara kwa mara, inapobidi ni chombo cha utekelezaji wa maamuzi yanayopitishwa na Bodi ya Huduma ya Afya ya Halmashauri. Timu hii pia itatoa ushauri wa kitaalam kwa Bodi.

2.4.4 Uhusiano na Sekta zingine kama vile Elimu na Maji

- Kamati ya Halmashauri ya Huduma za Jamii hupitisha mipango yote na ripoti za utekelezaji. Hivyo, Kamati hii itawezesha kuwepo kwa uhusiano wa sekta mbalimbali katika Halmashauri.
- Ushirikiano wa karibu na sekta zingine utazingatiwa na Bodi ya Huduma ya Afya ya Halmashauri kwenye maeneo yaliyopewa kipaumbele na yanayohitaji jitihada za pamoja katika utekelezaji wa mpango wa maendeleo wa Halmashauri.

2.4.5 Uhusiano na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Watoa Huduma Binafsi na Wahisani.

- Wajumbe wanaowakilisha, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na watoa huduma binafsi kwenye Bodi za Huduma za Afya za Halmashauri, watakuwa kiungo muhimu cha uhusiano na mashirika yao.
- Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya itahakikisha ushirikishwaji wa washika dau wote katika kuandaa mipango ya afya ya mwaka. Timu hii itawasilisha mipango hii kwa Bodi.
- Bodi ya Huduma ya Afya ya Halmashauri itatafuta fedha kutoka sehemu mbalimbali ikiwa ni pamoja na Halmashauri/ Serikali Kuu, Mashirika ya Hiari, Jamii na Wahisani.

2.4.6 Uhusiano na Halmashauri

- Bodi ya Huduma ya Afya ya Halmashauri itawajibika kwa Halmashauri.
- Taarifa za Mwaka za Mipango ya Afya ya Halmashauri, fedha na utekelezaji zitapitiwa na Kamati ya Huduma za Jamii, Kamati ya Mipango na Fedha na kuidhinishwa na Kikao cha Halmashauri.
- Bodi itaendesha shughuli zake kwa namna ambayo itaongeza zaidi ufanisi wa Halmashauri na vyombo vyake. Halmashauri haitaingilia mamlaka ya utendaji wa shughuli za kila siku za Bodi.

2.4.7 Uhusiano na Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Mkoa

- Timu ya Afya ya Mkoa itatoa msaada na ushauri wa kitaalamu unaohitajika na Bodi.

2.4.8 Uhusiano wa Bodi na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Wizara ya Afya

- Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Afya, zitatoa msaada wa kitaalamu kwa Bodi za Huduma za Afya za Halmashauri katika uandaaji wa sera, taratibu za kisheria, na kufuatilia shughuli za Bodi za Huduma za Afya za Halmashauri (Kifungu cha 174A na 54A cha Sheria ya Serikali za Mitaa na.7 na 8/1982).

2.5 USIMAMIZI WA RASILIMALI

2.5.1 Usimamizi wa fedha

- Kutakuwa na akaunti moja ya huduma za afya (akaunti namba 6). Akaunti itaendeshwa kwa kufuata kanuni za fedha za Serikali za Mitaa na itakuwa na wawekaji sahihi kama itakavyoonyeshwa mara kwa mara kwenye miongozo ya fedha.
- Bodi ya Huduma ya Afya ya Halmashauri itakuwa na akaunti ya Mfuko wa Afya ya Jamii. Akaunti hii itatunza fedha zinazotokana na mauzo ya kadi za wanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii na itatunza ada ya watumiaji huduma kutoka kwenye vituo vya huduma vya Halmashauri. Akaunti itatumika kuchangia fedha kwenye akaunti namba 6 ya Halmashauri katika kugharamia huduma za afya.
- Wawekaji saina akaunti namba 6 ni kama ifutavyo:

Kundi A: Mganga Mkuu wa Wilaya/Mji/Manispaa/Jiji au badili yake/msaidizi wake.

Kundi B: Mkurugenzi wa Halmashauri au badili yake/msaidizi wake.

- Wawekaji saina wa akaunti ya Mfuko wa Afya ya Jamii ni kama ifuatavyo:-
 - Kundi A – Mwenyekiti wa Bodi na mjumbe mmoja wa Bodi.
 - Kundi B – Katibu wa Kamati ambaye ni Mganga Mkuu wa Wilaya/Mji Manispaa/ Jiji au Mweka Hazina wa Halmashauri.
- Sahihi mbili ni budi zipatikane endapo fedha zinatolewa. Sahihi moja lazima itoke kwenye kundi A na nyingine kwenye kundi B. Benki haitakubali hundi iliyosainiwa na waweka saina wawili kutoka kundi moja tu.
- Halmashauri itateua wahasibu wawili ambao watahusika na akaunti za afya chini ya Mganga Mkuu wa Wilaya/Manispaa/Miji/Jiji.
- Mganga Mkuu wa Wilaya/Manispaa /Mji/Jiji atawajibika na uandaaji wa hati zote za malipo.
- Vyanzo vya fedha
 - Michango ya watu binafsi
 - Mfuko wa Afya ya Jamii
 - Ada za watumiaji huduma
 - Makusanyo ya fedha ya Halmashauri
 - Wahisani
 - Ruzuku toka Serikali Kuu

- Vyanzo vingine vya mapato

2.5.2 Usimamizi wa watumishi

- Bodi ya Afya itaishauri Halmashauri kuhusu ajira, maendeleo, mafunzo, motisha na mgawanyo wa watumishi wa afya.

2.5.3 Usimamizi wa vifaa

- *Uboreshaji wa miundombinu*

Bodi ya Huduma ya Afya ya Halmashauri itahakikisha upatikanaji wa miundombinu ya kutosha kwa kufanya matengenezo, ukarabati wa majengo yaliyopo na ujenzi wa majengo mapya pale inapolazimu.

- *Uboreshaji wa mahitaji*

Bodi ya Huduma ya Afya ya Halmashauri itahakikisha upatikanaji wa mahitaji muhimu kama dawa na vitendea kazi vya kitaalamu katika ngazi zote za huduma za afya.

- *Uboreshaji wa usafiri na mfumo wa uendeshaji.*

Bodi ya Huduma ya Afya ya Halmashauri itahakikisha kuwa usafiri wa kuaminika unakuwepo, mifumo na matengenezo yanafanyika palepanapohitajika.

2.6 MAJUKUMU YA BODI

Bodi ya Huduma ya Afya itahakikisha :

2.6.1 Jamii inapata huduma bora za afya inazozimudu, na zinazoimarisha afya zao.

2.6.2 Upatikanaji wa rasilimali na mgawanyo wake kwa kuzingatia mahitaji ya ngazi zote za huduma na matumizi bora .

2.7 KAZI ZA BODI

Bodi

2.7.1 Itajadili na kurekebisha mipango ya afya na bajeti na kuiwasilisha kwa Halmashauri kwa ajili ya kuidhinishwa;

2.7.2 Itapokea, kuchambua na kuidhinisha taarifa za utekelezaji kutoka kwa Timu za Uendeshaji wa Huduma za Afya za Halmashauri;

- 2.7.3 Itabuni vyanzo mbalimbali vya mapato na kukusanya rasilimali za kutosha kuendesha huduma za afya za Halmashauri;
- 2.7.4 Itaisaidia Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri katika kusimamia rasilimali za afya;
- 2.7.5 Itashirikiana na Kamati za Afya za Vituo na washirika wengine kwa nia ya kuinua kiwango cha afya na utoaji wa huduma;
- 2.7.6 Itaratibu na kusimamia shughuli za maendeleo ya afya katika eneo la mamlaka husika;
- 2.7.7 Itaimarisha miundombinu endelevu na mfumo wa mawasiliano na usambazaji.
- 2.7.8 Itahakikisha kunakuwepo wafanyakazi kulingana na ikama ya Halmashauri.

2.8 UWAJIBIKAJI

Bodi itawajibika kwa Halmashauri (ya Wilaya/Miji/Manispaa/Jiji).

Kumbuka: Uwajibikaji una maana ya mmiliki aliye na uwezo wa kuajiri, kufukuza au kuondoa, wajumbe na watumishi. Pia kusimika au kuvunja Bodi au Kamati.

2.9. UHALALI WA KISHERIA, MAMLAKA NA MIPAKA YA BODI

2.9.1 Utaratibu wa kisheria

Bodi za Huduma za Afya za Halmashauri zimeundwa chini ya sheria zifuatazo:-

- Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka ya Wilaya) ya Mwaka 1982;
- Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka ya Miji) ya Mwaka 1982;
- Hati rasmi (“Instrument”) iliyopitishwa na Halmashauri husika.

2.9.2 Mikataba ya fedha:

Bodi itahakikisha kuwa mikataba inasainiwa na mamlaka husika na itafuatilia utekelezaji wa mikataba hiyo.

2.9.3 Mamlaka na mipaka

- Hatua kwa hatua, Bodi itakuwa na wajibu na mamlaka kamili juu ya utawala na uendeshaji wa huduma za afya za Halmashauri.
- Bodi itakuwa na uhusiano wa kiutendaji na Kamati za Usimamizi za Vituo vya Huduma lakini hazitaingilia mfumo wa maamuzi yao mradi zinafanya kazi kwa kufuata miongozo na sera.
- Bodi haitaingilia mambo ya kiutaalamu ya watumishi mradi yako katika mipaka ya maadili ya kikazi.
- Wajumbe wa Bodi watafanya kazi kwa muda wa miaka 3 na wanaweza kuchaguliwa tena kwa awamu nyingine ya miaka 3.
- Kama mjumbe wa Bodi ameamua kujiuzulu atalazimika kutoa notisi ya mwezi mmoja.
- Endapo mjumbe wa Bodi atajiuzulu au atafariki, nafasi wazi itajazwa na mjumbe aliyechaguliwa kwa kipindi kilichobaki.
- Kama Bodi itashindwa kutimiza majukumu yaliyotarajiwa kama ilivyoainishwa na Hati rasmi (Instrument), Halmashauri itaivunja Bodi na kuandaa uchaguzi mwingine mara moja.
- Bodi itakutana mara nne kwa mwaka au wakati wowote inapolazimu.
- Idadi ya wajumbe wanaotakiwa katika mkutano itafikiwa wakati asilimia 50 ya wajumbe waliochaguliwa wanapohudhuria akiwemo Mwenyekiti au Katibu.

2.10 UTARATIBU WA KUPOKEA NA KUTOA TAARIFA

2.10.1 Taarifa kwa Bodi

Bodi itapokea taarifa zifuatazo:

- Taarifa ya Mipango ya Afya ya Halmashauri inayojumuisha Mipango ya Afya ya Kata na ya Vituo vya Huduma ambayo ni pamoja na shughuli zote za afya katika eneo husika;
- Taarifa za utekelezaji na fedha za kila robo mwaka na za mwaka zinazohusu mipango na hali ya afya kwa ujumla katika Halmashauri.

2.10.2 Taarifa kwa Halmashauri

Halmashauri itapokea yafuatayo kutoka Bodi ya Huduma ya Afya:-

- Mpango wa Afya wa Halmashauri
- Taarifa za utekelezaji na fedha za kila robo mwaka, na za mwaka ikiwa ni pamoja na taarifa kuhusu hali ya afya katika Halmashauri;

Kumbuka:

- Halmashauri itapeleka nakala halisi za taarifa kwa Sekretarieti ya Mkoa na nakala kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mkoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Afya.
- Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri inapovunjwa au kumaliza kipindi chake itakasimu madaraka yake kwa Timu ya Uendeshaji Huduma za Afya ya Halmashauri.
- Kwa upande wa Bodi /Kamati za Manispaa tatu za Temeke, Ilala na Kinondoni, kwa vile zinasimamia “Bamako Initiatives” inapidi kabla ya kumaliza muda wake, kuidhinisha asilimia 15 ya fedha ili Timu za Uendeshaji wa Huduma za Afya zilizokasimiwa madaraka ziweze kuendesha shughuli za “Bamako Initiatives” mpaka Bodi/Kamati mpya zitakapoingia madarakani.

3.0 TIMU YA UENDESHAJI WA HUDUMA ZA AFYA YA HALMASHAURI

3.1 WAJUMBE WA TIMU WATAKUWA KAMA IFUATAVYO:

1. Mganga Mkuu wa Wilaya/Manispaa/Mji/Jiji
2. Katibu wa Afya wa Wilaya/Manispaa/Mji/Jiji
3. Muuguzi Mkuu wa Wilaya/Manispaa/Mji/Jiji
4. Mfamasia wa Wilaya/Manispaa/Mji/Jiji
5. Afisa Afya wa Wilaya/Manispaa/Mji/Jiji
6. Fundi Sanifu wa Maabara wa Wilaya/Manispaa/Mji/Jiji
7. Daktari wa Meno wa Wilaya/Manispaa/Mji/Jiji

3.2 SIFA ZA WAJUMBE WA KAMATI

Sifa za wajumbe zitakuwa sawa na zile ambazo zimeelezwa katika kitabu cha “Organizational Structure, Job descriptions, Roles and Functions of RHMTs, CHMTs and HMTs in relation to CHSBs”.

3.3 TARATIBU ZA UTEUZI

Uteuzi wao utafuata taratibu za kiutawala za serikali na ni kulingana na sifa walizonazo.

3.4 UHUSIANO KATI YA JAMII, WASHIKA DAU NA MAMLAKA ZINGINE

3.4.1 Uhusiano na Jamii

Timu ya Uendeshaji Huduma za Afya ya Halmashauri itahakikisha kwamba jamii inashirikishwa kikamilifu katika kutambua matatizo, kuweka kipaumbele, kupanga, kuchangia huduma, kufuatilia na kutathmini utoaji wa huduma za afya.

3.4.2 Uhusiano na vituo vya kutolea huduma za afya

Mojawapo wa shughuli za Timu ya Uendeshaji Huduma za Afya ni kusimamia vituo vya afya na zahanati; kwa hiyo Timu hii itawasiliana na Kamati za vituo hivyo na kutoa ushauri na inapobidi kutoa maelekezo ya kuinua utoaji wa huduma za afya.

3.4.3 Uhusiano na Timu ya Uendeshaji Huduma za Afya ya Mkoa

Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri itakuwa inapeleka taarifa za utekelezaji na mipango kabambe ya afya kwa Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Mkoa kupitia Halmashauri husika na kupokea ushauri wa kitaalamu kutoka Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Mkoa kuhusu namna ya kuboresha huduma za afya katika Halmashauri.

3.4.4 Uhusiano na Sekta zingine kama vile Elimu na Maji

Timu ya Uendesaji Huduma za Afya ya Halmashauri itashirikiana na sekta zingine kama Elimu na Maji katika kuinua huduma za afya za Halmashauri zinazohusiana na elimu ya afya kwa jamii na utumiaji wa maji safi na salama.

3.4.5 Uhusiano na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Watoa Huduma Binafsi na Wahisani.

Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri inaweza kualika mjumbe kutoka Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuhudhuria kati ya mikutano yake inapobidi.

3.4.6 Uhusiano na Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri

Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri itakuwa inatekeleza shughuli zote ambazo zimeamuliwa na Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri.

3.4.7 Uhusiano na Halmashauri

Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri itakuwa inapokea maelekezo ya utekelezaji kutoka Halmashauri kwa kupitia Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri.

3.5 USIMAMIZI WA RASILIMALI

Usimamizi wa rasilimali utafuata taratibu za fedha za Halmashauri zilizopo.

3.6 MAJUKUMU NA KAZI ZA TIMU YA UENDESHAJI WA HUDUMA ZA AFYA YA HALMASHAURI

1. Kuandaa mipango kabambe ya afya ambayo inatilia mkazo mahitaji yote ya afya ya halmashauri kwa kuzingatia Mwongozo wa Kitaifa wa Wilaya wa Mipango ya Afya.
2. Kuhakikisha kuwa hospitali, vituo vya afya na zahanati zinatekeleza shughuli za afya na jamii inamiliki rasilimali kama inavyoelekeza mpango kabambe wa Afya wa halmashauri.
3. Kuhakikisha upatikanaji wa usafiri, dawa muhimu, chanjo, madawa, vifaa vya tiba, vifaa na kemikali za maabara katika hospitali, vituo vya afya na zahanati.
4. Kuwa tayari kukabiliana na magonjwa ya milipuko, maafa na kupanga mipango ya kudhibiti na kuzuia.

5. Kuhakikisha kuwa watumishi wa afya walioko katika ngazi mbalimbali kwenye halmashauri wanapata nyenzo za kuwawezesha kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za afya.
6. Kuhakikisha kuwa huduma za afya zitolewazo zinalingana na viwango vya kitaifa.
7. Kuhakikisha kuwa halmashauri inazingatia na kufuata sheria zilizowekwa, kanuni, maadili ya kitaaluma, na mwenendo wa tabia wa viongozi na watumishi.
8. Kuhakikisha kuwa watumishi wa afya wanakusanya takwimu, wanazichambua, wanazitumia katika mipango, wanatekeleza mipango hiyo na wanatoa mshindonyuma.
9. Kutambua maeneo ya kipaumbele, kusimamia na kufanya utafiti wa utendaji kazi katika halmashauri
10. Kujumuisha na kuchambua taarifa za utekelezaji na fedha za robo mwaka na mwaka halafu kuziwasilisha kwa Bodi ya Afya ya Halmashauri na Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Mkoa.
11. Kusimamia mikutano ihusuyo wataalamu wa afya wanaotoa huduma za afya kwenye halmashauri ili kuweza kutambua na kuratibu shughuli zote za afya.
12. Kusimamia na kusaidia huduma za afya ambazo zipo nje na mbali kutoka vituo vya kutolea huduma za afya (“outreach services”).
13. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa shughuli za afya kwenye halmashauri.

3.7 UWAJIBIKAJI

Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri itawajibika kwa Halmashauri.

3.8 UHALALI WA KISHERIA, MAMLAKA NA MIPAKA

Timu ya Uendeshaji wa huduma za afya ya Halmashauri inaundwa na:

- Sheria ya Serikali za Mitaa ya 1982 (Mamlaka ya Wilaya)
- Sheria ya Serikali za Mitaa ya 1982 (Mamlaka ya Mji)
- Hati rasmi iliyotungwa na kupitishwa na Halmashauri husika

3.9 MIKATABA YA FEDHA

Timu ya Uendeshaji Huduma za Afya ya Halmashauri itasimamia mikataba ya Kamati za Vituo (ikiwa ipo), imesainiwa kikamilifu na inafuatwa.

3.10 UTARATIBU WA KUPOKEA NA KUTOA TAARIFA

3.10.1 Kwa Timu ya Uendeshaji Huduma za Afya ya Mkoa

Itapeleka taarifa za utekelezaji na fedha za robo mwaka na za mwaka pamoja na mpango kabambe wa afya wa Halmashauri. Pia itapata mshindo nyuma na ushauri kuhusiana na uboreshaji wa huduma za afya katika Halmashauri.

3.10.2 Kwa Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri

Bodi itapokea kutoka Timu ya Uendeshaji Huduma za Afya ya Halmashauri:

- Mpango kabambe wa afya wa Halmashauri unaojumuisha mipango ya afya ya kata na ya vituo vya huduma.
- Taarifa za utekelezaji na fedha za kila robo mwaka na za mwaka zinazohusu mipango na hali ya afya kwa ujumla katika Halmashauri.

4.0 KAMATI YA USIMAMIZI WA HOSPITALI

4.1 WAJUMBE WA KAMATI YA USIMAMIZI WA HOSPITALI

4.1.1 Wajumbe wa Kamati ya Usimamizi wa Hospitali watakuwa katika makundi mawili:-

▪ Wajumbe wa kuchaguliwa (wanaopiga kura)	
- Watumiaji wa huduma za hospitali (jamii)	3
- Wajumbe kutoka Kamati za Vituo vya Afya na za Zahanati ..	2
- Mjumbe kutoka Huduma za afya Binafsi kwa faida ...	1
- Mjumbe kutoka Huduma za afya Binafsi bila faida	1
▪ Sekretarieti (wasiopiga kura)	
Hawa ni pamoja na:-	
- Mjumbe kutoka Bodi ya Huduma ya Afya ya Halmashauri	1
- Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya/Manispaa/Jiji(Katibu)	1
- Ofisi ya Mganga Mkuu wa Wilaya/Manispaa/Mji/Jiji.....	1
Jumla.....	10

Kumbuka:

- 1: Mwenyekiti wa kamati atachaguliwa miongoni mwa wajumbe wa kuchaguliwa. Anatakiwa asiwe mtumishi wa serikali aliyeajiriwa na halmashauri ya wilaya/manispaa/mji/Jiji.
- 2: Mganga Mfawidhi ataandamana na wakuu wa idara za hospitali wanaotakiwa wakati wa kuhudhuria mkutano wa Kamati ya Usimamizi ya Hospitali.
 - Kamati ya Usimamizi ya Hospitali itakuwa na hiari ya kumkaribisha mtu yeyote kuhudhuria kikao kama kutakuwa na ulazima.
- 3: Idadi ya wajumbe wanawake isipungue theluthi moja ya wajumbe wote. Pale ambapo idadi hiyo haitimii, nafasi hizo zitatangazwa tena na baada ya hapo wasipokatikana kigezo cha kuteua kitatumika.
- 4: Kamati inaweza kumteua mtaalamu yeyote ahudhurie pale utaalamu wake unapohitajika.

4.2 SIFA ZA WAJUMBE WA KAMATI

Sifa za wajumbe wa Kamati ya usimamizi ya Hospitali zitazingatia mambo makuu matatu:-

4.2.1 Umri

Kwa kuzingatia kazi za kamati, umri unaopendekezwa utakuwa kati ya miaka 21 na 65.

4.2.2 Uraia

Wajumbe wanaowakilisha watumiaji wa huduma na Kamati za Usimamizi za hospitali za vituo vya serikali watakuwa raia wa Tanzania, lakini hii haitakuwa lazima kwa wajumbe kutoka Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

4.2.3 Elimu:

Waombaji wanatakiwa kuwa wamehitimu elimu ya sekondari na kuendelea.

Kumbuka: Wajumbe wote wa kuchaguliwa hawatakiwi kuwa na wadhifa wowote wa kisiasa kupitia chama chochote cha siasa na wasiwe waajiriwa wa Halmashauri husika.

4.3 TARATIBU ZA UCHAGUZI

Wajumbe wa Kamati ya Usimamizi ya Hospitali watachaguliwa kwa utaratibu ufuatao:

- **Kutangaza nafasi wazi**

Mkurugenzi wa Halmashauri atatangaza nafasi wazi kwa ajili ya uwakilishi wa watumiaji huduma na vituo vya huduma za afya vya umma. Pia atahakikisha mawasiliano na umoja wa watoa huduma binafsi na Mashirika yasiyo ya kiserikali yanafanyika.

- **Maombi ya watu binafsi na uchaguzi**

Maombi na uchaguzi wa wajumbe utafanyikia kwenye kijiji au mtaa na kusimamiwa na Afisa Mtendaji wa Kijiji katika Halmashauri ya Wilaya au Afisa Mtendaji wa Kata katika Halmashauri ya Mji/Manispaa/Jiji. Uchaguzi utafanyika kwa njia ya mkutano wa hadhara na atachaguliwa mjumbe mmoja.

Baada ya uchaguzi, orodha ya wajumbe waliochaguliwa yatachambuliwa na Timu ya Uendeshaji ya Huduma za Afya ya Halmashauri. Mara baada ya uchambuzi yatapelekwa kwa Timu ya Uendeshaji ya Halmashauri.

- **Uchaguzi wa mwisho**

Uchaguzi mkuu wa wajumbe waliochaguliwa na kijiji/mtaa utafanywa Kikao Kikuu cha Halmashauri kupitia Kamati ya Huduma za Jamii baada ya kupendekezwa na Timu ya Uendeshaji ya Halmashauri.

Wawakilishi wa vituo vya afya na zahanati watachaguliwa na Timu ya Uendeshaji ya Huduma za afya ya Halmashauri na kupitishwa na Halmashauri.

- **Uzinduzi rasmi**

Kamati ya Usimamizi ya Hospitali itazinduliwa rasmi kwa ushuhuda wa Mkuu wa Wilaya baada ya kuidhinishwa na kikao kikuu cha Halmashauri husika.

4.4 UHUSIANO WA KAMATI NA JAMII, WASHIKA DAU NA MAMLAKA MBALIMBALI.

Uhusiano na Jamii	<input type="checkbox"/> Jamii inawakilishwa katika Kamati ya Usimamizi ya Hospitali ili kuhakikisha kuwa mahitaji ya Jamii yanashughulikiwa
Uhusiano na Timu ya Uendeshaji Huduma za Afya ya Halmashauri	<input type="checkbox"/> Timu ya Uendeshaji Huduma za Afya ya Halmashauri itatoa ushauri wa kitaalamu kwa Kamati ya Usimamizi wa Hospitali
Uhusiano na Bodi ya Huduma ya Afya ya Halmashauri	<input type="checkbox"/> Kamati inawakilishwa katika bodi ya afya ya Halmashauri. <input type="checkbox"/> Kamati ya Usimamizi ya Hospitali itapeleka mpango wa mwaka wa huduma za afya za hospitali na taarifa za utekelezaji na fedha za kila robo mwaka na mwaka kwa Bodi ya Huduma ya Afya ya Halmashauri.
Uhusiano na Sekta zingine	<input type="checkbox"/> Kamati ya Fedha na Mipango ya Halmashauri ina wajumbe kutoka sekta mbalimbali ambayo hupitisha mpango wa hospitali. Kamati hii itaboresha mahusiano kissekta.
Uhusiano na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Watoa Huduma binafsi na wahisani	<input type="checkbox"/> Itajenga na kuimarisha ushirikiano, na Mashirika, Watoa Huduma Binafsi na Wahisani kwa lengo la kuleta maendeleo ya hospitali.
Uhusiano na Timu ya Uendeshaji ya Hospitali	<input type="checkbox"/> Timu ya Uendeshaji ya Hospitali inatekeleza maamuzi yaliyofanywa na Kamati ya Usimamizi ya Hospitali
Uhusiano na Kamati za Afya za Vituo vya Huduma (Zahanati na Vituo vya Afya).	<input type="checkbox"/> Kamati za Vituo vya Afya na za Zahanati zinawakilishwa kwenye Kamati ya Usimamizi ya Hospitali ya Halmashauri.

4.5 USIMAMIZI WA RASILIMALI

4.5.1 Usimamizi wa fedha

Kutakuwa na akaunti moja ya Hospitali itakayohifadhi fedha za “user fees”. Akaunti itaendeshwa kwa kufuata kanuni za fedha za Serikali za Mitaa zilizopo na kutakuwa na waweka sahihi kama itakavyoainishwa mara kwa mara kwenye miongozo ya fedha.

- Waweka saina akaunti ya hospitali watakuwa kama ifuatavyo:

Kundi A: Mganga Mfawidhi wa Hospitali au Katibu wa Afya

Kundi B: Mweka Hazina wa Halmashauri au Mganga Mkuu wa Wilaya/Mji/Manispaa/Jiji.

- Mganga Mkuu wa Wilaya/Manispaa/Miji/Jiji atamteua mmojawapo wa wahasibu wake kushughulikia uendeshaji wa akaunti ya hospitali chini ya Mganga Mfawidhi.
- Mganga Mfawidhi ataandaa hati zote za malipo zinazohusiana na shughuli za hospitali.
- Akaunti ya hospitali itakaguliwa kwa kuzingatia taratibu za serikali.
- **Vyanzo vya fedha**
 - Michango binafsi
 - Uchangiaji Huduma za Afya.
 - Makusanyo ya fedha za Halmashauri
 - Wahisani
 - Ruzuku kutoka Serikali Kuu
 - Vyanzo vingine vya mapato.

4.5.2 Usimamizi wa watumishi

Kamati ya Usimamizi ya Hospitali itaishauri Halmashauri kuhusu ajira, maendeleo, mafunzo, motisha, na mgawanyo wa watumishi wa afya.

4.5.3 Usimamizi wa vifaa

- **Uboreshaji wa miundombinu**

Kamati ya Usimamizi ya Hospitali itahakikisha upatikanaji wa miundombinu ya kutosha kwa kufanya matengenezo, ukarabati wa majengo yaliyopo na ujenzi wa majengo mapya inapolazimu.

- **Upatikanaji wa mahitaji muhimu**

Kamati ya Usimamizi ya Hospitali itahakikisha upatikanaji wa mahitaji yote muhimu kama dawa na vitendea kazi vya kitaalamu katika hospitali.

- **Uboreshaji wa usafiri na mfumo wa uendeshaji**

Kamati ya Usimamizi ya Hospitali itahakikisha kuwa usafiri, vifaa, mawasiliano vinakuwepo na mfumo wa matengenezo unafuatwa.

4.6 MAJUKUMU YA KAMATI

Kamati ya Usimamizi ya Hospitali itahakikisha

- kuwa wakazi wanapata huduma za afya zinazostahili na wanazozimudu,
- upatikanaji wa rasilimali za kutosha kuendeshea huduma za hospitali.

4.7 KAZI ZA KAMATI

Kamati ya Usimamizi ya Hospitali

- 4.7.1** Itapokea, itachambua, itarekebisha na itapitisha mipango ya hospitali kutoka Timu ya Uendeshaji ya Hospitali.
- 4.7.2** Itapokea na kujadili taarifa za utekelezaji za kila robo mwaka na za mwaka zilizoandaliwa na Timu ya Uendeshaji ya Hospitali.
- 4.7.3** Itabuni vyanzo mbalimbali vya mapato na kukusanya rasilimali za kutosha kuendesha huduma za Hospitali.
- 4.7.4** Itashirikiana na kamati zingine za afya na washirika mbalimbali katika utoaji na uboreshaji huduma za afya.
- 4.7.5** Itaimarisha miundombinu endelevu na mfumo wa mawasiliano na usambazaji huduma za afya.
- 4.7.6** Itahakikisha kunakuwepo wafanyakazi kulingana na ikama ya hospitali husika.
- 4.7.7** Kwa kupitia wajumbe wake itahakikisha kuwa jamii inapatiwa maelezo ya uhakika kuhusu mipango na maendeleo ya uendeshaji huduma za afya katika hospitali.

4.8 UWAJIBIKAJI

Kamati ya Usimamizi ya Hospitali itawajibika kwa Halmashauri husika na itakuwa na uhusiano wa kiutendaji na Bodi ya Huduma ya Afya ya Halmashauri. Kamati hii itakuwa inapeleka taarifa za utekelezaji za robo mwaka na mwaka na mpango wa hospitali kwa Bodi ya Huduma za afya ya Halmashauri.

4.9 UHALALI WA KISHERIA, MAMLAKA NA MIPAKA YA KAMATI YA USIMAMIZI YA HOSPITALI

Utaratibu wa kisheria	<p>Kamati za Usimamizi za Hospitali zinaundwa chini ya sheria zifuatazo:-</p> <ul style="list-style-type: none"> <input type="checkbox"/> Sheria ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 6 Kifungu cha 86A na 52A – 1999. <input type="checkbox"/> Hati rasmi (“Instrument”) iliyotungwa na Halmashauri husika.
Mamlaka na mipaka ya kamati	<ul style="list-style-type: none"> <input type="checkbox"/> Hatua kwa hatua Kamati za Usimamizi za Hospitali zitakuwa na mamlaka kamili juu ya utawala na uendeshaji huduma za hospitali. <input type="checkbox"/> Kamati za Usimamizi hazitaingilia mambo ya kitaalamu ya wafanyakazi.
Kipindi cha kuwa madarakani	<ul style="list-style-type: none"> <input type="checkbox"/> Uchaguzi mkuu utafanyika kila baada ya miaka mitatu. <input type="checkbox"/> Wajumbe wa Kamati za Usimamizi za Hospitali watafanya kazi kwa vipindi viwili vya miaka mitatu mitatu. <input type="checkbox"/> Mwenyekiti wa kamati atatoka miongoni mwa wajumbe waliochaguliwa. <input type="checkbox"/> Kama mjumbe ameamua kujiuzulu, atatakiwa kutoa notisi ya mwezi mmoja. <input type="checkbox"/> Endapo mjumbe wa kamati atajiuzulu au kufariki, nafasi wazi itajazwa na mjumbe aliyechaguliwa kwa kipindi kilichobaki. <input type="checkbox"/> Kama kamati itashindwa kutimiza majukumu yaliyotarajiwa kama ilivyoainishwa na Hati rasmi; Halmashauri itaivunja Kamati na kufanya uchaguzi mwingine mara moja.
Mikutano	<ul style="list-style-type: none"> <input type="checkbox"/> Kamati itakutana mara nne kwa mwaka na wakati mwingine wowote inapolazimu. <input type="checkbox"/> Idadi ya wajumbe wa mkutano itakuwa imekamilika wakati asilimia 50 ya wajumbe waliochaguliwa wanapohudhuria akiwemo Mwenyekiti au Katibu.

4.10 MIKATABA YA FEDHA

- Kamati ya Usimamizi ya Hospitali itahakikisha kwamba mikataba ya fedha inasainiwa sawasawa na mamlaka zinazohusika na itafuatilia utekelezaji wa mikataba hiyo.

4.11 UTARATIBU WA KUPOKEA NA KUTOA TAARIFA

- Timu ya Uendeshaji Huduma za Afya ya Hospitali itapeleka taarifa ya Mpango wa Afya wa Hospitali pamoja na taarifa za utekelezaji na fedha za kila robo mwaka na za mwaka kwa Kamati ya Usimamizi ya Hospitali.
- Taarifa hizo zitawasilishwa kwa Bodi ya Huduma ya Afya ya Halmashauri kupitia Timu ya Uendeshaji Huduma za Afya ya Halmashauri.

Kumbuka: Kamati ya Usimamizi ya Hospitali ikivunjwa au kumaliza kipindi chake, itakasimu madaraka yake kwa Timu ya Uendeshaji Huduma za Afya ya Hospitali.

5.0 KAMATI YA KITUO CHA AFYA

5.1 WAJUMBE WA KAMATI

5.1.1 Wajumbe wa Kamati ya Kituo cha Afya watakuwa katika makundi mawili:-

- **Wajumbe wa kuchaguliwa (wanaopiga kura):-**
 - Watumiaji wa huduma za kituo, watakaochaguliwa mmoja kutoka kila Kata - 3
 - Mjumbe kutoka Kamati za Zahanati (kwa kupokezana)- 1
 - Mjumbe kutoka Umoja wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali- 1
 - Mjumbe kutoka Huduma za Afya Binafsi Bila faida - 1
 - Mjumbe kutoka Huduma za Afya Binafsi kwa faida - 1
- **Sekretariati (wasiopiga kura)**
 - Mjumbe kutoka Kamati ya Maendeleo ya Kata (kwa kupokezana)- 1
 - Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya atakuwa Katibu wa kamati- 1

Jumla ya wajumbe = 8

Kumbuka: - Wajumbe wanaowakilisha watumiaji wa huduma watabadilishana baada ya kipindi cha miaka mitatu kumalizika ili kuruhusu ushirikishwaji wa jamii katika uendeshaji huduma za afya za kituo.

- Idadi ya wajumbe wanawake isipungue theluthi moja ya wajumbe wote. Pale ambapo idadi hiyo haitimii, nafasi hizo zitatangazwa tena na baada ya hapo wasipopatikana kigezo cha kuteua kitatumika.
- Wajumbe wa kupokezana kutoka Kamati za Zahanati au Kamati ya Maendeleo ya Kata itafanyika kila mwaka. Dondoo za vikao zitakuwa zinapelekwa kwa wajumbe wote wa Kamati za Zahanati, za Maendeleo za Kata na kwa mwaka kutafanyika mikutano miwili ambayo itawahusisha wajumbe wote wa Kamati za Zahanati na Maendeleo za Kata.

5.2 SIFA ZA WAJUMBE WA KAMATI YA KITUO CHA AFYA

Sifa za wajumbe wa Kamati ya Kituo cha Afya zitazingatia mambo yafuatayo:-

5.2.1 Umri:

Kwa kuzingatia kazi za wajumbe wa Kamati ya Afya, umri utakuwa kati ya miaka 21 na kuendelea.

5.2.2 Uraia

Wajumbe watakaowakilisha jamii wanatakiwa kuwa raia wa Tanzania. Hii siyo lazima kwa watakaowakilisha Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali.

5.2.3 Elimu:

Wawe waliomaliza elimu ya msingi au zaidi na wajue kusoma na kuandika “Kiswahili” vizuri. Vinginevyo watu wanaojua kusoma na kuandika na wenye uzoefu na sifa za uongozi zinazokubalika watafikiriwa pia.

Kumbuka: Wajumbe wote wa kuchaguliwa hawatakiwi kuwa na wadhifa wowote wa kisiasa kupitia chama chochote cha siasa wala wasiwe waajiriwa wa Halmashauri husika.

5.3 UTARATIBU WA UCHAGUZI WA WAJUMBE

Utaratibu utakuwa kama ifuatavyo:-

5.3.1 Matangazo

Afisa Mtendaji wa Kata kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya/ Manispaa/Mji, atatangaza nafasi wazi kwa ajili ya wawakilishi wa watumiaji huduma na wale wa vituo vya afya na zahanati. Pia atahakikisha mawasiliano na Mashirika yasiyo ya kiserikali yatoayo huduma za afya katika eneo husika.

5.3.2 Maombi kutoka kwa watu binafsi na uchaguzi wa awali

- Maombi na uchaguzi wa wajumbe utafanyikia kwenye kijiji au mtaa na kusimamiwa na Afisa Mtendaji wa Kijiji katika Halmashauri ya Wilaya au Afisa Mtendaji wa Kata katika Halmashauri ya Mji/Manispaa/Jiji. Uchaguzi utafanyika kwa njia ya mkutano wa hadhara na atachaguliwa mjumbe mmoja.
- Orodha ya wajumbe waliochaguliwa yatachambuliwa na Timu ya Uendeshaji ya kila kata kabla ya kuwasilishwa kwa Kamati ya Maendeleo ya Kata ambapo Kituo cha Afya kipo.

5.3.3 Uchaguzi wa mwisho

- Uchaguzi mkuu utafanyika kila baada ya miaka mitatu kwa kuzingatia taratibu zote zilizokubalika.
- Kamati ya Maendeleo ya Kata ambapo Kituo cha Afya kipo itafanya uchaguzi mkuu wa wajumbe wa Kamati na kuwasilisha orodha yao kwa Kikao Kikuu cha Halmashauri kwa kuidhinishwa.

- Halmashauri itarejesha orodha ya wajumbe walioidhinishwa kwa Kamati ya Maendeleo ya Kata.

5.3.4 Uzinduzi rasmi

Uzinduzi wa Kamati ya Kituo cha Afya utafanywa na Kamati ya Maendeleo ya Kata ambapo kituo cha Afya kipo na kushuhudiwa na Mwenyekiti wa Halmashauri.

5.4 UHUSIANO WA KAMATI YA KITUO CHA AFYA, JAMII , WASHIKA DAU NA MAMLAKA ZINGINE

Uhusiano na Jamii	<ul style="list-style-type: none"> ❑ Jamii inawakilishwa katika Kamati ya Kituo cha Afya ili kuhakikisha matakwa ya Jamii yanafanyiwa kazi.
Uhusiano na Timu ya Uendeshaji Huduma za Afya ya Halmashauri	<ul style="list-style-type: none"> ❑ Timu ya Uendeshaji Huduma za Afya ya Halmashauri itatoa ushauri wa kitaalamu kwa Kamati ya Kituo cha Afya
Uhusiano na Bodi ya Huduma ya Afya ya Halmashauri	<ul style="list-style-type: none"> ❑ Kamati ya Kituo cha Afya itapeleka Mpango wa Mwaka wa Huduma za Afya za Kituo na taarifa za utekelezaji na fedha za kila robo mwaka na mwaka kwa Bodi ya Huduma ya Afya ya Halmashauri. ❑ Kamati ya Kituo cha Afya itawakilishwa kwenye Bodi ya Huduma ya Afya ya Halmashauri ili kuhakikisha kuwa mambo yanayohusu Kituo cha Afya yanafanyiwa kazi.
Uhusiano na Timu ya Uendeshaji ya Kituo cha Afya	<ul style="list-style-type: none"> ❑ Timu ya Uendeshaji Huduma za Afya ya Kituo cha Afya itatoa ushauri wa kitaalamu kwa Kamati ya Kituo cha Afya na itatekeleza maamuzi ya kamati.
Uhusiano na sekta zingine.	<ul style="list-style-type: none"> ❑ Kamati ya fedha na mipango ina wajumbe kutoka sekta mbalimbali ambayo hupitisha mipango ya kituo cha Afya kama sehemu ya mpango wa afya wa Halmashauri. ❑ Wajumbe wa Timu ya Uendeshaji ya Kata na Kamati ya Maendeleo ya Kata watajenga na kuimarisha mahusiano ya kissekta kupitia mjumbe wa kamati ya kituo.
Uhusiano na Mashirika	<ul style="list-style-type: none"> ❑ Kamati ya Kituo cha Afya itatafuta fedha kutoka vyanzo

yasiyo ya Kiserikali. Watoa Huduma Binafsi na Wahisani	mbalimbali. ❑ Mahusiano yataboreshwa kupitia kwa wajumbe wote husika kutoka Umoja wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali.
Uhusiano na Kamati ya Zahanati	❑ Kamati ya zahanati inawakilishwa kwenye Kamati ya Kituo cha Afya.

5.5 USIMAMIZI WA RASILIMALI

5.5.1 Usimamizi wa fedha

- Fedha kwa ajili ya uendeshaji wa Kituo cha Afya zitasimamiwa na Mganga Mkuu wa Wilaya kupitia akaunti na. 6. Hata hivyo, Vituo vya Afya vilivyoko maeneo ya mjini vinaweza kufungua akaunti tofauti mahali inapothibitika kwamba kuna ulazima. Hii itategemea kiasi cha fedha katika mzunguko.
- Pale ambapo Kituo cha Afya katika maeneo ya mjini kitalazimika kuwa na akaunti tofauti, itabidi Halmashauri iajiri mhasibu wa kuhudumia akaunti hiyo.
- Mkuu wa Kituo cha Afya kilichoko mjini/manispaa/jiji ataandaa hati zote za malipo zinazohusu kituo cha afya.
- Kamati itahakikisha kuwa Kituo cha Afya kina chumba na sanduku madhubuti kwa ajili ya kuhifadha fedha.
- Akaunti ya Kituo cha Afya itakaguliwa kwa mujibu wa kanuni za fedha za serikali za mitaa.
- Vyanzo vya fedha
 - Michango binafsi
 - Wahisani/washirika
 - Ruzuku ya Halmashauri husika
 - Mfuko wa Afya ya Jamii
 - Ruzuku kutoka Serikali Kuu
 - Vyanzo vingine

5.5.2 Usimamizi wa watumishi

- Kamati ya Kituo cha Afya itaishauri Halmashauri kwa kupitia Timu ya Uendeshaji Huduma za Afya ya Halmashauri na Bodi ya Huduma ya Afya ya

Halmashauri kuhusu ajira, mafunzo, mgawanyo, motisha na maendeleo ya watumishi.

5.5.3 Usimamizi wa vifaa

- *Uboreshaji wa miundombinu*

Kamati ya Kituo cha Afya itahakikisha upatikanaji wa miundombinu endelevu ya kutosha ya Kituo cha Afya kwa kufanya matengenezo, ukarabati wa majengo yaliyopo na ujenzi wa majengo mapya inapobidi.

- *Uboreshaji wa mahitaji muhimu*

Kamati ya Kituo cha Afya itahakikisha upatikanaji wa mahitaji muhimu kama vile dawa na vifaa vingine vya kitaalamu.

- *Uboreshaji wa usafiri na mfumo wa uendeshaji.*

Kamati ya Kituo cha Afya itahakikisha kuwa usafiri, mifumo ya uendeshaji, mawasiliano, nyumba za watumishi, matengenezo vinakuwepo na vinafanya kazi ipasavyo.

5.6 MAJUKUMU YA KAMATI

Kamati ya kituo ch afya itahakikisha

5.6.1 kuwa wakazi wa eneo husika wanapata huduma za afya zinazostahili na wanazozimudu.

5.6.2 kuwepo kwa rasilimali za kutosha za kuendeshea huduma za kituo

5.7 KAZI ZA KAMATI

Kamati

5.7.1 Itapokea, itachambua na itapitisha mipango na bajeti ya Kituo cha Afya.

5.7.2 Itapokea taarifa ya utekelezaji na ya fedha ya kila robo mwaka na ya mwaka iliyoandaliwa na Timu ya Uendeshaji ya Kituo cha Afya.

5.7.3 Itabuni vyanzo mbalimbali vya mapato na kukusanya rasilimali za kutosha kuendeshea huduma za Kituo cha Afya.

5.7.4 Itashirikiana na Bodi ya Huduma ya Afya na washirika mbalimbali katika utoaji na uboreshaji wa huduma za afya.

- 5.7.5** Itaimarisha miundombinu endelevu na mfumo wa mawasiliano na usambazaji wa huduma za afya.
- 5.7.6** Itashauri na kutoa mapendekezo kwa Halmashauri kuhusu watumishi katika nyanja za ajira , mgawanyo, mafunzo, maendeleo na motisha .
- 5.7.7** Itaisaidia Timu ya Uendeshaji ya Kituo cha Afya katika kupanga na kusimamia mambo ya afya ya Jamii katika eneo lake kama sehemu ya Mpango wa Maendeleo wa Kata.

5.8 UWAJIBIKAJI

Kamati ya Afya ya Kituo itawajibika kwa Halmashauri ya Wilaya/Mji/Manispaa/ Jiji husika.

5.9 UHALALI WA KISHERIA, MAMLAKA NA MIPAKA YA KAMATI YA KITUO

Taratibu za kisheria	<p>Kamati ya Kituo inaundwa chini ya Sheria zifuatazo:-</p> <ul style="list-style-type: none"> <input type="checkbox"/> Sheria ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982 kama ilivyorekebisha na Sheria Namba 6 Kifungu cha 86A na 52A – 1999. <input type="checkbox"/> Hati rasmi (“Instrument”) iliyotungwa na Halmashauri husika.
Mamlaka na mipaka ya Kamati.	<ul style="list-style-type: none"> <input type="checkbox"/> Hatua kwa hatua Kamati ya Kituo cha Afya itakuwa na wajibu na mamlaka kamili juu ya utawala na uendeshaji wa huduma za afya za Kituo. <input type="checkbox"/> Kamati ya Kituo cha Afya haitaingilia mambo ya kitaalam ya watumishi.
Kipindi cha kuwa madarakani	<ul style="list-style-type: none"> <input type="checkbox"/> Wajumbe wa Kamati ya Kituo cha Afya watafanya kazi kwa vipindi viwili vya miaka mitatu mitatu. <input type="checkbox"/> Mwenyekiti wa kamati atatoka miongoni mwa wajumbe waliochaguliwa. <input type="checkbox"/> Kama mjumbe ameamua kujiuzulu, atatakiwa kutoa notisi ya mwezi mmoja. <input type="checkbox"/> Endapo mjumbe wa kamati atajiuzulu au kufariki, nafasi wazi itajazwa na mjumbe aliyechaguliwa kwa kipindi kilichobaki. <input type="checkbox"/> Kama Kamati ya Kituo cha Afya itashindwa kutimiza majukumu yaliyotarajiwa, kama ilivyoainishwa kwenye Hati rasmi; Halmashauri itaivunja kamati na kufanya uchaguzi mwingine mara moja.

Mikutano	<ul style="list-style-type: none"> ❑ Kamati itakutana mara nne kwa mwaka au wakati mwingine wowote inapolazimu. ❑ Idadi ya wajumbe wa mkutano itakuwa imetimia endapo asilimia 50 ya wajumbe waliochaguliwa watahudhuria akiwemo Mwenyekiti au Katibu.
----------	--

5.10 MIKATABA YA FEDHA

- Kamati itahakikisha kuwa mikataba ya Kituo cha Afya inasainiwa vizuri na mamlaka zinazohusika na zinafuata makubaliano.

Kumbuka: Kamati ya Kituo cha Afya inapovunjwa au kumaliza kipindi chake itakasimu madaraka yake kwa Timu ya Uendeshaji Huduma za Afya ya Kituo cha Afya.

6.0 KAMATI YA AFYA YA KATA

6.1 WAJUMBE WA KAMATI

Wajumbe wa Kamati hii watakuwa wana uhusiano wa karibu na sheria ya Mfuko wa Afya ya Jamii ya mwaka 2001. Kwa hiyo kamati hii itakuwa na wajumbe wafuatao:

- 1) Diwani wa Kata ambapo ina kituo cha huduma za afya.
- 2) Afisa Mtendaji wa Kata
- 3) Mwalimu Mkuu mmoja kutoka shule ya msingi ambayo ipo kwenye Kata, ambaye atateuliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata.
- 4) Wajumbe wawili kutoka kwa Jamii, mmojawapo ni lazima awe mwanamke.
- 5) Tabibu au Afisa Tabibu Mfawidhi wa Kituo cha huduma za Afya, ambaye atakuwa Katibu wa Kamati.
- 6) Mjumbe mmoja aliyeteuliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata ambaye atatokana na wajumbe ambao wamependekezewa na wanakijiji wanaoishi kwenye kata husika na
- 7) Mwakilishi mmoja wa Jamii ambaye atateuliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata.

Mwenyekiti na Naibu Mwenyekiti wa Kamati atachaguliwa kutokana na wajumbe wa Kamati.

6.2 SIFA ZA WAJUMBE

Sifa za Kamati ya Afya ya Kata zitazingatia mambo matatu:

6.2.1 Umri

Umri utakuwa kuanzia miaka 21 hadi 65.

6.2.2 Uraia

Raia wa Tanzania (Mtanzania)

6.2.3 Elimu

Elimu ya Msingi au zaidi na awe anaelewa kusoma na kuandika kiswahili. Vinginevyo, mtu mzima mwenye sifa za uongozi zinazokubalika atafikiriwa.

6.3 TARATIBU ZA UCHAGUZI

Taratibu zitafuata uanachama wao, lakini Afisa Mtendaji wa Kata atasimamia utaratibu wa kuwapata.

6.4 UHUSIANO WA KAMATI NA JAMII, WASHIKADAU NA MAMLAKA ZINGINE

6.4.1 Kwa Jamii

Kamati itahusika na uhamasishaji na kuandaa jamii iwe tayari katika kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii.

6.4.2 Kwa Kamati ya Kituo cha Huduma za Afya

Kutoa/kupeleka taarifa muhimu zinazohusu masuala ya Mfuko wa Afya ya Jamii.

6.4.3 Kwa Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri

Kupeleka taarifa za utekelezaji na fedha za robo mwaka na mwaka za Mfuko wa Afya ya Jamii kutoka kwenye eneo husika.

6.5 USIMAMIZI WA RASILIMALI

Hakuna usimamizi wa moja kwa moja isipokuwa utakuwa ni ule wa kusimamia wakusanyaji wa fedha za Mfuko wa Afya ya Jamii.

6.6 KAZI

Kazi za Kamati ya Afya ya Kata zitakuwa:

6.6.1 Kukusanya na kuandaa jamii wawe wajumbe wa Mfuko wa Afya ya Jamii.

6.6.2 Kuandaa orodha ya wajumbe na kufuatilia idadi ya wajumbe kwenye jamii.

6.6.3 Kusimamia Wakusanyaji wa michango ya mwaka.

6.6.4 Kusimamia michango na mapato ya fedha za kuchangia huduma.

6.6.5 Kupitia utendaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii na kutoa mapendekezo na ufumbuzi.

6.6.6 Kuanzisha na kuratibu mipango ya afya ya Jamii na;

6.6.7 Kusimamia mikutano ya wajumbe wa Mfuko wa Afya ya Jamii.

Kumbuka: Mipango ya afya ya jamii inamaanisha mipango kabambe ya afya ya kata.

6.7 UWAJIBIKAJI

Kamati itawajibika kwa Halmashauri.

6.8 UHALALI WA KISHERIA, MAMLAKA NA MIPAKA YA KAMATI

Kamati ya Afya ya Kata inaundwa na:

- Sheria ya Mfuko wa Afya ya Jamii ya 2001
- Hati rasmi iliyopitishwa na Halmashauri husika.
- Kipindi cha kuwa madarakani: Wajumbe wa Kamati kila mmoja atafanya kazi kwa kipindi cha miaka mitatu na anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu.

6.9 UTARATIBU WA KUPOKEA NA KUTOA TAARIFA

6.9.1 Kwa Kamati ya Kituo cha Afya

Kamati ya Afya ya Kata itapeleka mpango kabambe wa afya na taarifa za utekelezaji na fedha za robo mwaka na mwaka kwa Kamati ya Kituo cha Afya.

6.9.2 Kwa Kamati ya zahanati

Kamati ya Afya ya Kata itapokea mipango kabambe ya afya na taarifa za utekelezaji na fedha za robo mwaka na mwaka kutoka Kamati ya zahanati.

7.0 KAMATI YA ZAHANATI

7.1 WAJUMBE WA KAMATI

▪ Waliochaguliwa (watakaopiga kura)				
- Watumiaji huduma za zahanati -	3
- Mwakilishi kutoka Huduma za afya Binafsi kwa faida			1
- Mwakilishi kutoka Huduma za afya Binafsi bila faida			1
▪ Sekretarieti (wasiopiga kura)				
- Mwakilishi kutoka Kamati ya Maendeleo ya Kata		1
- Mwakilishi kutoka Kamati ya Serikali ya Kijiji –		1
- Mganga Mfawidhi wa Zahanati (Katibu) –	1
Jumla.....	8

Kumbuka:

Idadi ya wajumbe wanawake isipungue theluthi moja ya wajumbe wote. Pale ambapo idadi hiyo haitimii, nafasi hizo zitatangazwa tena na baada ya hapo wasipopatikana kigezo cha kuteua kitatumika.

7.2 SIFA ZA WAJUMBE

Sifa za wajumbe wa Kamati ya Zahanati zitazingatia mambo matatu:-

7.2.1 Umri

Kwa kuzingatiaa kazi za wajumbe wa kamati, umri unaopendekezwa ni kuanzia miaka 21 hadi 65.

7.2.2 Uraia

Mwakilishi wa watumiaji huduma ni budi awe raia wa Tanzania. Hii sio lazima kwa mjumbe anayewakilisha Umoja wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali.

7.2.3 Elimu

Mjumbe wa kamati anatakiwa awe amehitimu elimu ya msingi au zaidi na lazima ajue kusoma na kuandika angalau “kiswahili”. Vinginevyo, mtu mzima mwenye sifa za uongozi zinazokubalika atafikiriwa.

Kumbuka: Wajumbe wote wa kuchaguliwa hawatakiwi kuwa na nyadhifa zozote za kisiasa kwa kupitia chama chochote cha siasa wala wasiwe waajiriwa wa Halmashauri husika.

7.3 TARATIBU ZA UCHAGUZI

- Afisa Mtendaji wa Kata kwa niaba ya Mkurugenzi wa Wilaya/ Manispaa/Mji /Jiji atatangaza nafasi wazi kwa wawakilishi wa watumiaji wa zahanati na pia kwa Mashirika yasiyo ya kiserikali.
- Maombi na uchaguzi wa wajumbe utafanyikia kwenye kijiji au mtaa na kusimamiwa na Afisa Mtendaji wa Kijiji katika Halmashauri ya Wilaya au Afisa Mtendaji wa Kata katika Halmashauri ya Mji/Manispaa/Jiji. Uchaguzi utafanyika kwa njia ya mkutano wa hadhara na atachaguliwa mjumbe mmoja.
- Orodha ya wajumbe waliochaguliwa itapelekwa kwa Kamati ya Maendeleo ya Kata kwa ajili ya uchaguzi mkuu/mwisho baada ya kuchambuliwa na Timu ya Uendeshaji ya Kata.
- Orodha ya wajumbe waliochaguliwa itapelekwa kwa Halmashauri ili kuidhinishwa.
- Halmashauri baada ya uteuzi itarudisha majina ya wanakamati kwa Kamati ya Maendeleo ya Kata.
- Kamati ya Maendeleo ya Kata itazindua Kamati ya Zahanati ikishuhudiwa na Diwani.

7.4 UHUSIANO WA KAMATI YA ZAHANATI NA JAMII, WASHIKA DAU NA MAMLAKA ZINGINE

Uhusiano na Jamii	<ul style="list-style-type: none"> ❑ Jamii zinachangia kutoa wajumbe kwenda kwenye Kamati ya Zahanati ili kuhakikisha kuwa mahitaji ya Jamii yanashughulikiwa ❑ Kamati ya Zahanati itaboresha mawasiliano kati ya watoa huduma na jamii yenye lengo la kuboresha huduma zenyewe.
Uhusiano na Timu ya Uendeshaji Huduma za Afya ya Halmashauri.	<ul style="list-style-type: none"> ❑ Timu ya Uendeshaji Huduma za Afya ya Halmashauri itatoa ushauri wa kitaalamu kwa Kamati za Zahanati.
Uhusiano na Bodi za Huduma ya Afya za Halmashauri	<ul style="list-style-type: none"> ❑ Kamati ya Zahanati itawakilishwa katika Bodi ya Huduma ya Afya ya Halmashauri ili kuhakikisha kuwa mambo ya zahanati yanashughulikiwa. ❑ Kamati za Zahanati zitawakilishwa katika mtindo wa kubadilishana ❑ Kamati ya Zahanati itapeleka taarifa za maendeleo za kila robo mwaka, na za mwaka ili kupitiwa na bodi.

Uhusiano na Timu ya Uendeshaji ya Zahanati	<input type="checkbox"/> Timu ya Uendeshaji ya Zahanati inatekeleza maamuzi ya Kamati ya Zahanati.
Uhusiano wa sekta zingine	<input type="checkbox"/> Itashirikiana na sekta zingine katika mambo yanyohitaji nguvu ya pamoja kuleta maendeleo ya zahanati.
Uhusiano na Kamati ya Kituo cha Afya	<input type="checkbox"/> Kamati ya Zahanati inawakilishwa katika Kamati ya Kituo cha Afya
Uhusiano na Mashirika yasiyo ya kiserikali na binafsi	<input type="checkbox"/> Kamati itajenga na kuimarisha ushirika kwa lengo la kukuza raslimali za maendeleo ya Zahanati.

7.5 USIMAMIZI WA RASILIMALI

7.5.1 Usimamizi wa fedha:

- Fedha kwa ajili ya uendeshaji wa Zahanati zitasimamiwa na Mganga Mkuu wa Wilaya kupitia akaunti na. 6. Hata hivyo, Zahanati zilizoko maeneo ya mijini/manispaa/jiji zinaweza kufungua akaunti tofauti mahali inapothibitika kwamba kuna ulazima. Hii itategemea kiasi cha fedha katika mzunguko.
- Mganga Mfawidhi wa zahanati iliyoko mjini/manispaa/jiji ataandaa hati zote za malipo zinazohusiana na zahanati
- Kamati itahakikisha kuwa zahanati ina chumba maalum na sanduku madhubuti kwa usalama wa kutunzia fedha.
- Akaunti za zahanati zitakaguliwa kwa mujibu wa kanuni za fedha za serikali
- Vyanzo vya fedha
 - Michango binafsi.
 - Ada za watumiaji huduma/uchangiaji huduma za Afya utakapoanza mfuko wa Afya ya Jamii (CHF)
 - Fedha za Halmashauri yenyewe
 - Wahisani/washirika
 - Serikali Kuu
 - Vyanzo vingine

7.5.2 Usimamizi wa Wafanyakazi

- Kamati ya Zahanati itaishauri Halmashauri husika kuhusu maendeleo ya watumishi katika nyanja za ajira, mafunzo, mgawanyo, maendeleo na motisha.

7.5.3 Usimamizi wa vifaa

- *Uboreshaji wa miundombinu*

Kamati itahakikisha upatikanaji wa miundombinu ya kutosha ya Zahanati kwa kufanya matengenezo, ukarabati wa majengo yaliyopo na kujenga mapya inapobidi.

- *Upatikanaji wa mahitaji muhimu*

Kamati ya Zahanati itahakikisha upatikanaji wa mahitaji muhimu kama vile dawa, kemikali na vifaa vya kitaalam.

- *Uboreshaji wa usafiri na mfumo wa uendeshaji:*

Kamati itahakikisha kuwa usafiri; mifumo ya matengenezo, mawasiliano na nyumba za wafanyakazi vinakuwepo na vinafanya kazi ipasavyo.

7.6 MAJUKUMU YA KAMATI

Kamati itahakikisha

- Kuwa wakazi katika eneo lake la kisheria wanapata huduma za afya zinazostahili na wanazozimudu.
- Kunakuwepo na raslimali za kutosha na wakati wowote kwa ajili ya huduma za zahanati.

7.7 KAZI ZA KAMATI

Kamati

7.7.1 Itapokea, itajadili na itapitisha mipango na bajeti ya zahanati.

7.7.2 Itapokea taarifa za utekelezaji zilizotayarishwa na Timu ya Uendeshaji ya Zahanati.

7.7.3 Itatambua na kutafuta rasilimali za kifedha za kuendesha huduma za zahanati.

7.7.4 Itashirikiana na Bodi zingine za Afya na washirika wengine katika utoaji na uendelezi wa huduma.

7.7.5 Itaendeleza miundombinu ya afya endelea na mgao wa uhakika wa mahitaji muhimu na mfumo wa mambo muhimu.

7.7.6 Itashauri na kupendekeza kuhusu masuala ya watumishi yanayohusu ajira, mafunzo, mgawanyo, maendeleo na motisha.

7.7.7 Itaisaidia Timu ya Uendeshaji ya Zahanati kupanga na kusimamia shughuli mbalimbali za Jamii katika eneo lake kuhusu Mipango ya Maendeleo ya Kata.

7.8 UWAJIBIKAJI

Inawajibika kwa halmashauri husika.

7.9 UHALALI WA KISHERIA, UPEO WA MAMLAKA NA MIPAKA

Chombo cha kisheria	<input type="checkbox"/> Sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 kama ilivyorekebishwa na Sheria Namba C sehemu ya 86 A na 52 – 1999 <input type="checkbox"/> Hati rasmi (“Instrument”) iliyoundwa na Halmashauri moja moja.
Mamlaka na mipaka ya kamati	<input type="checkbox"/> Hatua kwa hatua Kamati ya Zahanati itakuwa na mamlaka kamili juu ya utawala na uendeshaji wa huduma za afya za zahanati. <input type="checkbox"/> Kamati ya Zahanati haitaingilia masuala ya kitaalamu ya watumishi.
Muda wa kazi	<input type="checkbox"/> Wajumbe wa Kamati ya Zahanati watafanya kazi kwa kipindi cha miaka 3 lakini wanaweza kuomba kuchaguliwa tena kwa vipindi. <input type="checkbox"/> Mwenyekiti wa kamati atachaguliwa miongoni mwa wajumbe waliochaguliwa . <input type="checkbox"/> Kama mjumbe atajiuzulu au kufariki nafasi wazi itajazwa na mjumbe aliyechaguliwa kwa muda uliosalia. <input type="checkbox"/> Endapo Kamati ya Zahanati itashindwa kutimiza majukumu yaliyotarajiwa, Halmashauri itaivunja Kamati ya Zahanati na kufanya uchaguzi mpya.
Mikutano	<input type="checkbox"/> Kamati ya Zahanati itakutana mara nne kwa mwaka au inapobidi kufanya hivyo. <input type="checkbox"/> Idadi ya wajumbe wa mkutano itakuwa imetimia wakati asilimia 50 ya wajumbe waliochaguliwa watahudhuria akiwemo Mwenyekiti na/au Katibu

7.10 MIKATABA YA FEDHA

Kamati ya Zahanati itahakikisha kuwa mikataba imesainiwa na Mamlaka husika na itafuatilia makubaliano.


Kumbuka: Kamati ya Zahanati inapovunjwa au kumaliza kipindi chake itakasimu madaraka yake kwa Timu ya Uendeshaji Huduma za Afya ya Zahanati.

- Kumbuka:**
1. *Mwongozo huu, unafuta miongozo ya awali kuhusu uanzishaji wa Bodi za Huduma za Afya na Kamati za Ushauri za Hospitali mbalimbali kama vile Kamati ya ushauri ya Hospitali juu ya uchangiaji wa huduma za afya na Mfuko wa Afya ya Jamii.*
 2. *Pia mwongozo huu, hauzuii wataalamu wa afya kufanya kazi zao kama ilivyoelekezwa kwenye majukumu yao ya kazi.*


8.0 Viambatanisho:

Kiambatanisho I

**NAFASI YA BODI YA HUDUMA YA AFYA YA HALMASHAURI KATIKA MUUNDO WA TAASISI WA HUDUMA ZA AFYA
KITAIFA**



NAFASI YA BODI YA AFYA YA HALMASHAURI KATIKA MUUNDO WA HALMASHAURI



Kiambatanisho III**ORODHA YA WASHIRIKI**

NA.	JINA	CHEO	ANUANI
1	Dr. F. Njau	Head, HSR Secretariat, MoH	Box 9083, Dar es Salaam
2	Dr. R.B. Kalinga	Head, District Health Services	Box 9083, Dar es Salaam
3	Maximmillian Mapunda	Head, SWAp/BF	Box 9083, Dar es Salaam
4.	Dr. A. Hingora	Head, HSPS	Box 9083, Dar es Salaam
5	R. Shirima	CHF Consultant	Box 9083, Dar es Salaam
6	J.A. Kelya	Administrator, HSRS	Box 9083, Dar es Salaam
7	J.B. Rugo	PORALG	Box 1923, Dodoma
8	R.D. Mutagwaba	Health Planner, Kinondoni Municipal cOUNCIL	Box 61665, Kinondoni MC, D'Salaam
9	Dr. K.S. Ikamba	Medical Officer of Health	Tanga Municipal Council
10	Dr. Oberlin M.E. Kisanga	National Co-ordinator DHSP	Box 65350,D'Salaam
11	Dr. E. Nangawe	Head, Health, CSSC	Box 9433, Dar es Salaam
12	Dr. A. Ole'Sulul	RMO, Kagera Region	Box 265, Kagera
13	C.N. Hamza	Health Secretary, Office of CMO	Box 9083, Dar es Salaam
14	B.L. Nallya	Health Administrator, Ilala MC	Box 25411, Ilala M.C.
15	R.J. Mninoi	Personnel Officer	Box 9083, Dar es Salaam
16	L. Masayanyika	DMO, Temeke M.C.	Box 45232, Temeke M.C.
17	C.M. Kahwa	Health Secretary	Box 265, Bukoba
18	Ms. D. Mbuya	Asst. Quality Ass. Officer	Box 9083, Dar es Salaam
19	Ms. A. Lukwatage	H.Resource Devt. Officer	Box 265, Bukoba
20	Dr. Nkwera H.D.	Regional Medical Officer	Box 259, Mbeya
21	Mr. W.H. Kipigapasi	District Executive Director	Box 148, Tukuyu
22	R. Nsemwa	DPLO	Box 3, Mbozi
23	C.A. Kuhenga	Municipal Health Officer	Box 149, Mbeya
24	Dr. A.B.M. Gao	District Medical Officer	Box 70, Mbozi
25	Mr. A.A. Ngajilo	Head, CTU	Box 9083, Dar es Salaam
26	Ms. P. Maganga	Legal Officer, MoH	Box 9083, Dar es Salaam
27	Ms. Rose Shija	Quality Assurance Officer	Box 9083, Dar es Salaam

NA.	JINA	CHEO	ANUANI
28	F.D. Lubuva	Information Officer	Box 9142, Dar es Salaam
29	N.B. Mwamwaja	Health Promotion Specialist	Box 65219, Dar es Salaam
30	F.J. Masaule	Head, HSR Advocacy	Box 9083, Dar es Salaam
31	Ms. R. Kikuli	Head, Budget Section, MoH	Box 9083, Dar es Salaam
32.	Ms. A. Nswila	Admin, Preventive Serv. MoH	Box 9083, Dar es Salaam
33	Dr. P. Mbuji	Strategy Coordinator 7, MoH	Box 9083, Dar es Salaam
34.	J. Sendoro	Economist, MoH	Box 9083, Dar es Salaam
35.	S.A. Nzori	Parliamentary Draftman	Box 9050, Dar es Salaam
36.	Ms. Suzey Nipha	Accountant	Box 9083, Dar es Salaam
37.	Mr. E. Malamsha	Accountant	Box 9083, Dar es Salaam
38.	M. Jazza	Secretary, HSR Secretariat	Box 9083, Dar es Salaam
39.	E. Kawalega	Secretary, MOH	Box 9083, Dar es Salaam
40.	A. Kalewa	Accountant	Box 9083, Dar es Salaam

REJEA

1. The Local Government Laws (Miscellaneous Amendments Act, 1999) Act Supplement No. 5 of 16th April, 1999)
2. Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa mapitio ya marekebisho ya Sheria za Mtaa, Na. 6 ya Mwaka 1999 (January 2000).
3. Waraka wa Utumishi Na. 1 wa Mwaka 1999: Taratibu za Utendaji kazi katika muundo mpya wa Tawala za Mikoa Tanzania Bara.
4. Majaribio ya Mabadiliko ya Utoaji Huduma Bora ya Afya Kagera – Mada za maelekezo ya utendaji kazi – Bodi ya Afya ya Wilaya.
5. The status/position of the Kagera HSR Test Programme and District Health Boards Orientation Manual experiences learnt from the DSM reforms.
6. District Health Boards/Health Facility Committee Selection Guidelines manual, Nov. 1999.
7. Organisational structure, job descriptions, roles and functions of RHMTS DHMT and HMT in relation to the DHBs (September 1999).
8. District Health Boards Orientation Manual (August,1999).
9. The Tanga Municipal Council (Establishment of Municipal Health Fund) By Laws, 1999.
10. The Lushoto District Council (establishment of District Health Fund) By Laws, 1999.
11. The Lushoto District Council (establishment of District Health Fund By Laws, 1999.
12. Community Health Fund (CHF) Design 1999
13. Community Health Fund (CHF) Training Guidelines 1999.
14. Community Health Fund (CHF) District Health Plan Model. 1999
15. Community Health Fund (CHF) Operation Guidelines 1999
16. Local Government (District and Urban Authorities) Acts, 1982
17. Staffing levels for Health Facilities/Institutions; MOH/CSD April, 1999.